**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**HALMASHAURI MANISPAA YA SHINYANGA**


**SHULE YA SEKONDARI RAJANI**

**S.L.P 1107 – SHINYANGA**.

Nambaza simu:

Mkuu wa shule: **0765434965/0613671509**

Makamu Mkuu wa Shule; **0764594500/0629550494**

Mwalimu wa Taaluma; **0769158941**

Patron/Matron **0765133739/0766895696**


**08/05/2026**

Mzazi/Mlezi wa…………………………………………………………… ……

S.L.P……………………………………………………………………….

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI RAJANI HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA MKOA WA SHINYANGA</u>**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2026 chaguo la HGL, HGK, HGE, HKL na KLF – katika shule ya Sekondari Rajani Shinyanga iliyoko Mkoani Shinyanga. HONGERA SANA. Unatakiwa kufika hapa shuleni tarehe tajwa hapo chini na utapokelewa na Makamu Mkuu wa Shule pamoja na mwalimu wa zamu. Muhula wa masomo unaanza tarehe **……………..** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……………..** na mwisho wa kuripoti ni tarehe …………..

1. **USAFIRI:**

   Ufikapo mjini Shinyanga kama umeshukia kituo cha mabasi cha Shinyanga (Stendi ya Manyoni), panda pikipiki kwenda soko kuu shilingi 2,000/= ambapo utakuta hiace au bajaji nauli yake ni shilingi 1,500/= ziendazo Kolandoto shuka Rajani Sekondari.

2. **MAHALI SHULE ILIPO:**

   Shule hii ipo kulia kando ya barabara iendaya Mwanza, umbali wa kilometa 10 kutoka Shinyanga Mjini. Shule ipo mbele ya Kiwanda cha Jambo kwa wanaotokea mjini shinyanga.

## 3. MAHITAJI: _

### (a) VIFAA

Vifaa vifuatavyo ni vya lazima mwanafunzi kuja navyo shuleni.

- Godoro (futi 2½ upana) na foronya yake rangi ya pinki au bluu bahari.
- Ream 02 za karatasi za photocopy (Photocopy Paper A4) kwa mwaka mzima kwa ajili ya mitihani yake ya kila wiki, mwezi na muhula.
- Ndoo mbili (02) ndogo zenye mifuniko kwa ajili ya kuogea na kufulia
- Mto1 na foronya za rangi ya pinki zisizo na maua
- Shuka 2 za kulalia rangi ya pinki au bluu bahari na chandarua.
- Nguo za ndani za kutosha na mahitaji yake muhimu.
- Faili la kuhifadhi mitihani yake.
- Vyombo vya kulia chakula (kikombe,sahani,bakuli na kijiko)
- Blanket moja (la kawaida) **kwa wenye matatizo ya kiafya.**
- Daftari kubwa, counter book 8, kalamu za wino na penseli za kutosha.
- Scientific calculator (Casio Fx991,) kwa michepuo ya HGL, HGL, HGE na HGK
- Aje na mathematical set.
- Aje na vitabu vya masomo ya tahasusi (Combination) yake.
- Taulo za kike (kwa wasichana)
- Mopper mbili (2) kwa mwanafunzi

- Aje na vifaa vya usafi kwa mchanganuo ufuatao kulinganana michepuo yao

| NA. | TAHASUSI | KIFAA |
|---|---|---|
| 1 | HGK | Mfagio wa nje 01 na mopper 01 |
| 2 | HGL | JEMBE 01 NA MPINI 01 |
| 3 | HKL | Mopper 01na mfagio wa nje 01 |
| 4 | HGE | FYEKEO 01 |
| 5 | KLF | REKI 01 |

NB. Kutokana na umbali atokapo mwanafunzi, usumbufu wa kusafiri na mizigo mizito, anaweza kuja na kununulia baadhi ya mahitaji hapa shuleni mfano: (Reams, counter books Q4, mifagio, mpini, mopper, fyekeo na reki)

### (a) SARE ZA SHULE WASICHANA (UNIFORM):

- Sketi mbili (2) za rangi ugoro iliyoiva (dark coffe/dark snuff colour) ashone rinda box mbele na nyuma ivuke magoti na isiwe na urefu wakuburuzika kwa ajili ya darasani
- Gauni mbili (2) za dark blue zenye rinda box mbele na nyuma za kushindia. (Kitambaa cha Esteem)

- Juba/Shungi mbili nyeupe kwa Waislam zinazofunika kifua .
- Shati mbili nyeupe za tetroni, mikono mirefu kwa wakristo.
- Sweta ya ugolo
- Tai rangi ya rangi ya sketi, inapatikana shuleni
- Kizibao chenye rangi ya sketi.
- T –Shirt yenye kola dark blue inapatikana shuleni
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye kisigino kifupi, visiwe vimechongoka mbele na viwe vya kamba, jozi mbili.
- Soksi rangi nyeupe ndefu jozi 4.

**Nguo za michezo**

- Track suit rangi ya kijivu nzito (adibas)
- Raba nyeupe za kamba
- Jezi rangi ya timu ya taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes)
- Skin tight ndefu nyeusi

**(b) SARE ZA SHULE WAVULANA (UNIFORM):**

- Suruali mbili (02) za rangi ya Ugoro iliyoiva (dark coffe/dark snuff colour kwa ajili ya darasani
- Shati mbili nyeupe za tetroni, mikono mirefu
- Surual 02 dark blue kwa ajili ya kushindia. Ziwe na upana chini (18) na zisiwe za kubana.
- Sweta rangi ya ugolo
- Aje na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye kisigino kifupi, jozi moja au Zaidi.Viatu visiwe vimechongoka mbele na viwe vya kamba.
- Tai rangi ya suruali.
- Soksi rangi nyeusi jozi 02
- Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
- T-Shirt yenye kola rangi dark blue, inapatikana shuleni kwa Tsh.13,000/=

**Sare za michezo**

- Track suit rangi ya kijibu nzito (adidas)Tsh 20,000
- Jezi ya bluu - timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes)
- Aje na raba za michezo..

**MICHANGO MBALI MBALI**

| NA. | AINA YA MICHANGO | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | **Mchango wa uendeshaji wa shule** | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Hakikisha unalipia michango hiyo inalipiwa benki **(NMB, AC/NO: 30701100039– RAJANI SEKONDARY SCHOOL)** na usije na pesa za michango ya shule mkononi. Pay in slip (Risiti ya malipo ya benki) **iwe na majina ya mwanafunzi na sio ya Mzazi/Mlezi.**

**NB**:Mwanafunzi ajapo shuleni anatakiwa kuja na **Results lip** ya kidato cha nne na nakala ya **cheti cha kuzaliwa** (Birth

certificate)

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule ina endeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978. Unatakiwa kuzingatia (sheria) mambo ya msingi yafuatayo.


**BAADHI YA SHERIA ZA MSINGI NI:**

- Heshima kwa wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika shughuli zote za kila siku ndani na nje ya shule
- Kuzingatia kikamilifu mipaka ya shule na uwepo wa ndani ya mipaka hiyo wakati wote mwanafunzi akiwa shuleni.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani au nje ya shule kwa muda wote wa uanafunzi wako.
- Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- Kuvaa sare za shule wakati wote, mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi shuleni.
- Kuwahi katika shughuli zote za shule.
- Kuzingatia ratiba ya shule wa kati wote
- Kutokuleta radio,simu ya mkononi au card au charger ya simu shuleni, vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari. Mwanafunzi akikutwa na kitu kimoja wapo kati ya vitu hivyo adhabu yake ni kufukuzwa shule.
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini au kumshawishi mwenzake abadili dini wa wapo shuleni.
- Hairuhusiwi kutumia mshumaa au kibatari ila ataruhusiwa kumiliki taa inayotumia betri au solar

**MWISHO**

Unapo ripoti unatakiwa kukabidhi fomu ya ahadi ya mwanafun zina ahadi ya mzazi/mlezi pamoja na fomu ya uchunguzi wa afya kwa Makamu Mkuu wa shule.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI RAJANI**



GERALD PASCHAL MAJALIWA
**MKUU WA SHULE**

**NB**: Kwa siku za hivi kribuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa, mtoto wa mzazi wa mwanafunzi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO

| | |
|---|---|
| MKUU WASHULE | **0765434965/0613671509** |
| MAKAMU ,MKUU WA SHULE | **0764594500/0629550494** |
| MWALIMU WA TAALUMA | **0769158941** |

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA MASOMO AU KUFUKUZWA SHULE.**

- Wizi
- Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
- Kugoma na kuhamasisha mgomo
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwaUjumla.
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule,
- Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
- Kufuga ndevu
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- Uvutaji wa sigara
- Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- Kusababisha mimba
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- Kudharau Bendera yaTaifa
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi
- Kutoroka/ kulala nje ya shule bila ruhusa

**VIAMBATANISHO NA FOMUMUHIMU VYA KUJA NAVYO SHULENI.**

1. FOMUYA UCHUNGUZI WA AFYA (Ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali)
2. FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI/MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO , FUJO NA MAKOSA YA JINAI.
3. FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE.
4. PICHA 04 ZAWAZAZI/WALEZI NA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI PAMOJA NA NAMBA ZAO ZA

SIMU

**PMO - RALG**

Rajani Secondary School,

P.O.Box1107,

**SHINYANGA.**

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

This form must be completed by a government medical officer.

Student's Full Name: ………………………………………………………………………………..………..

Present age: ……………………………………………… Sex: ……………………..………………………

Blood test:………………………………………………Group:…………………………………….…………..

Stool Examination:………………………………………………………………………………………..……

T. S. Test: ……………………………………………………………………………………..………..……..

Asthma: ……………………………………………………………………………………………..……..

Eye disorder: …………………………………………………………………………………….………..

Nose disorder: ……………………………………………………………………………………………..

Ear disorder: ………………………………………………………………………………..………..

Skin disease: ………………………………………………………………………………………………..

Anemia: …………………………………………………………………………………………..……..

Chest: ……………………………………………………………………………………………….……..

Operations:……………………………………………………………………………...…………..

Serious accidents: ………………………………………………………………………..…………

Any other infection disease: ……………………………………………………………..………………

Pregnancy........................................................................................................... (In case of female)

ADDITIONAL INFORMATIO Ne.g.Physical defects of impairments chronic of family disease etc.

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………I

certify that I have personally examined Mr./Miss……………………………………………………..………

And found him/her/unfit to pursue further studies.

SIGNATURE:………………………………………

DESIGNATION:……………………………………

(Official rubber stamp)

STATION: ……………………………………………

DATE: ………………………………………………

**SHULE YA SEKONDARI RAJANI**

**FOMU YA KUKUBALI MWANAFUNZI**

(ijazwe kwa **herufi kubwa** na **irejeshwe** kwa mkuu wa shule)

1. Jinakamili:……………………………………………………………………………........................... Tarehe ya kuzaliwa:……………………Wilaya:……………………..Mkoa:………………….. Taifa: ……………………………………….. Dini: ……………………………………………..
2. Jina kamili la baba/mama/mlezi: ………………………………………………………..……….. Anwaniyake:……………………………………………………………………………..………… … Kazi ya baba/mama/mlezi:……………………………………………………………..………… Namba yasimu:……………………………………………………………………………..……

**AHADI YA MWANAFUNZI:**

(a) Mimi ……………………………………………nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha Tano katika shule ya Sekondari Rajani kuanzia tarehe......................................... hadi nitakapomaliza kidato cha sita.

(b) Kwahiyo naahidi kwamba;

(i) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.

(ii) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi washule na serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kama kushiriki migomo, fujo, makosa ya jina in.k.najua pia SIMU, UTORO na UCHELEWAJI shuleni HAVIKUBALIKI.

(iii) Nitatunza mali za umma ambazo ni pamoja na majengo, samani, vitabu n.k.

Tarehe:……………………………………..Sahihi ya mwanafunzi:………………………………….

Sahihi ya Dole gumba

**AHADIYAMZAZI/MLEZI:**

Mimi:……………………………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi

… ....................................................................... Naahidi kwamba;

1. Nitashirikiana na uongozi wa shule, walimu na watumishi wasio walimu katika kuhakikisha mwanangu anatii sheria na kanuni za shule ya Sekondari Old shinyanga. Iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimika kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongozi wa shule.
2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kusoma kwa kulipa ada na michango mingine kama ilivyoelekezwa na shule

   Sahihi:………………………… ….

   Tarehe:……………………… ……